# JAMHURI YA KENYA

## SERIKALI YA KAUNTI YA NAKURU

# MANISPAA YA GILGIL

# MKATABA WA HUDUMA

HARAMBEE

KAUNTI YA NAKURU

## SISI NI NANI

Manispaa ya Gilgil inapata mamlaka yake kutoka Katiba ya Kenya ya mwaka 2010, Sheria ya Miji na Maeneo ya Mijini, Sheria ya Serikali za Kaunti, Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sheria ya Afya ya Umma na majukumu mengine yaliyo kabidhiwa na Serikali ya Kaunti. Majukumu yetu ni pamoja na upangaji miji, udhibiti wa maendeleo, barabara, mifereji ya maji, taaake za barabarani, usimamizi wa taka, usimamizi wa mazingira, mbuga za umma, masoko, ukusanyaji wa mapato ya manispaa, utawala wa makazi, huduma kwa wateja na utawala wa manispaa.

## DIRA

Manispaa safi, jumuishi, yenye uchumi imara na yenye upangaji bora kwa mustakabali endelevu wa miji.

## DHAMIRA

Kutoa huduma bora, bunifu, jumuishi na endelevu za manispaa kupitia usimamizi madhubuti wa rasilimali, ushiriki wa wadau na ushirikiano wa kimkakati.

## MAADILI YA MSINGI

Uadilifu • Uwajibikaji • Utaalamu • Uwazi • Haki • Mteja Kwanza • Ubunifu • Kazi ya Pamoja
Ujumuishwaji • Utunzaji wa Mazingira • Ubora • Uwajibikaji wa Haraka

## LENGO KUU

Lengo kuu la idara hii ni kukakilisha kwamba makazi ya binadamu yanapangwa na kuhuduniwa vyema katika mazingira safi na yenye afya.

## MALENGO YA KIMKAKATI

- Kutoa huduma bora na zenye ufanisi za manispaa.
- Kukuza upangaji endelevu wa miji.
- Kuboresha kuridhika kwa wateja.
- Kuweka uwajibikaji na uwazi.
- Kuchochea ukuaji wa uchumi na uwekezaji.
- Kuboresha uhifadhi wa mazingira.
- Kukuza ushiriki wa umma.
- Kuboresha ufanisi wa taasisi.

| NA. | HUDUMA INAYOTOLEWA | MAHITAJI YA MTEJA | GHARAMA | MUDA WA KUKAMILISHA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Maswali na taarifa | Ziara ofisini, simu au ombi la maandishi | Bure | Moja kwa moja |
| 2. | Malalamiko na mrejesho | Suluhisho la malalamiko | Bure | Siku 7 |
| 3. | Usimanizi na kuthibitisha mawasiliano | Uthibitisho wa mawasiliano | Bure | Moja kwa moja |
| 4. | Ukusanyaji wa mapato | Majengo yaliyosajiliwa na malipo yanayotumika | Kulingana na Sheria ya Fedha za Kaunti | Inaendelea |
| 5. | Ukitangaza matangazo | Barua ya maombi, fomu | Kulingana na Sheria ya Fedha za Kaunti | Ndani ya siku 60 |
| 6. | Mapitio ya maombi ya ujenzi | • Uthibitisho wa umiliki<br>• Michoro ya usanifu iliyodhinishwa kikamilifu<br>• Uidhinishaji wa ardhi<br>• Michoro ya miundo<br>• Fomu za fidia za michoro | Kulingana na Sheria ya Fedha za Kaunti | Ndani ya siku 60 |
| 7. | Ukaguzi wa majengo | • Michoro ya usanifu iliyodhinishwa<br>• Michoro ya miundo iliyodhinishwa<br>• Fomu za fidia zilizodhinishwa | Kulingana na Sheria ya Fedha za Kaunti | Inaendelea |
| 8. | Maombi ya matengenezo ya barabara | Ombi la maandishi likionyesha eneo | Bure | Ukaguzi wa eneo ndani ya siku 7 za kazi |
| 9. | Maombi ya matengenezo ya mifereji | Malalamiko/ombi | Bure | Ukaguzi ndani ya siku 7 za kazi |
| 10. | Kuarifu hitilafu za taa za barabarani | Taarifa sahihi ya eneo | Bure | Ndani ya siku 7 za kazi |
| 11. | Mikutano ya ushiriki wa umma | Mahudhurio ya wadau | Bure | Kulingana na ratiba |
| 12. | Mchakato wa zabuni | • Kustahiki awali<br>• Zabuni<br>• Ufunguzi<br>• Tathmini<br>• Notisi | Bure | Ndani ya siku 30 |
| | | Kusaini mkataba | Bure | Siku 14 baada ya notisi ya tuzo |
| | | Makabidhiano ya tovuti | Bure | Siku 7 baada ya kusaini mkataba |
| | | Ukaguzi wa mradi | Bure | Inaendelea |
| | | Utoaji wa cheti cha ukamilishaji | Bure | Juma 1 baada ya ombi |
| | | Malipo | Bure | Wiki 4 |
| 13. | Maoni na pongezi | Fomu ya maoni, barua pepe au taarifa kwa mdomo | Bure | Utambuzi ndani ya siku 1 ya kazi na suluhisho ndani ya siku 14 za kazi |

## HAKI ZAKO KAMA MTEJA

- Kupata huduma bora na ya heshima;
- Kupata taarifa; kushiriki maamuzi;
- Kulipa kwa uwazi; kusikilizwa malalamiko yako;
- Kufikia huduma bila ubaguzi.

## WAJIBU WAKO KAMA MTEJA

- Kutoa taarifa sahihi; kuzingatia sheria na kanuni za manispaa;
- Kulipa ada zinazotumika; kuwasilisha hati kamili;
- Kudumisha usafi; kushiriki katika shughuli za umma;
- Kuripoti uharibifu wa miundombinu; kuheshimu na kutenda kwa heshima.

## KWA MASWALI / MALALAMIKO – WASILIANA NASI

**Meneja wa Manispaa, Manispaa ya Gilgii**
S.L.P. 2870 – GILGIL,
Simu: (051) 2214142
Barua pepe: gilgilmunicipalityboard@gmail.com
Tovuti: www.nakuru.go.ke

**Katibu wa Tume / Afisa Mkuu Mtendaji, Tume ya Utawala na Haki za Kijamii**
2nd floor, West End Towers, Waiyaki Way, Nairobi
S.L.P. 20414-00200 Nairobi
Simu: +254 (020) 2270000 / 2303000
Barua pepe: complain@ombudsman.go.ke

**HUDUMA BORA NI HAKI YAKO**